

سُنَّة ثَابِتَة - سَوْا حِيلَى ١٠٠

SUNNA 100 ZILIZO THIBITI



جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ . فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ .٠١٦


جمعية الدعوة بالإلزافي

SUNNA 100

ZILIZO THIBITI

١٠٠ سُنّة ثابتة - سواحيلي

Kimetafsiriwa na kuhakikiwa na:
Abubakar Kassimu Abubakar
Ally Nassoro Ally
Abdallah Ally Chumbe



جمعية الدعوة والرشاد ونوعية الطالبات في الزلفي
Tel: 966 164234466 - Fax: 966 164234477

UTANGULIZI

Kutoka kwa Abu Huraira – Allah amridhie - amesema: Mtume wa Allah- Rehema na Amani za Allah zimfikie- amesema -: "Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: Mwenye kumfanyia uadui ninae mpenda, basi mimi nimemtangazia vita. Na hatojikaribisha kwangu mja wangu kwa chochote ninacho kipenda zaidi ya kile nilicho mwajibishia kwake, na hatoacha mja wangu kujikurubisha kwangu kwa kufanya ibada za sunna mpaka nitampenda, na nikimpenda basi Mimi nitakuwa ndio masikio yake anayosikia kwayo. macho yake anayo ona, na mkono wake anaopiga nao, na mguu wake anaotembea nao, na akiniomba, nitampa, na akiniomba ulinzi wangu nitamlinda, Na sikusitasita juu ya chochote ambacho ningefanya, kama kusita kwangu juu ya roho ya Muumini, anachukia kifo nami ninachukia kufanya lilio baya kwake" [Bukhari: 6502]

Tanbihi: kusita hapa kwa Allah, sio kwa kuwa na mashaka na kitu au kuhofia kushindwa, bali ni huruma yake kwa mja wake.

SUNNA ZA KULALA

١ - النوم على وضوء: قال النبي - ﷺ - للبراء بن عازب رضي الله عنه: «إذا أتيت مضمجعك ، فتوضاً وضوءك للصلوة ، ثم اضطجع على شفك الأيمن ...

[الحديث] [متفق عليه: ٦٣١١ - ٦٨٨٢]

1- Kulala na udhuu:

Mtume -Rehema na Amani za Allah zimfikie-alimwambia Al-Baraa bin Azib -Allah amridhie-“Ukitaka kulala, tia udhu wako kama Uduh wako wa swala, kisha lala ubavu wako wa kulia... Hadithi” [Imekubaliwa na Bukhari na Muslim. 6311-6882]

٢ - التكبير والتسبيح عند النمام: عن علي رضي الله عنه، أن رسول الله - ﷺ - قال حين طلبت إليه فاطمة - رضي الله عنها - خادمًا: «ألا أدلّكما على ما هو خير لكم من خادم؟ إذا أويستما إلى فراشكما، أو أخذتما مسامعكم، فكبرا أربعًا وثلاثين، وسبحا ثلاثًا وثلاثين، واحمدا ثلثًا وثلاثين. فهذا خير لكم من خادم» [متفق عليه: ٦٣١٨ - ٦٩١٥]

2- KuletaTakbira na Tasbiha wakati wa kulala:

Imepokelewa na Ali –Allah amridhie-, kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu - Rehema na Amani za Allah zimfikie - alisema pale Faatimah -Mwenyezi Mungu amuwiye radhi- alipo muomba ampatie mtumishi: "Je, nisikuambie lililo bora kwako kuliko mtumishi? Mkilala, au Mkifika kitandani, basi semenii, 'Allahu Akbaru mara thelathini na nne', na Subhaana llah mara thelathini na tatu, na Alhamdu lillahi mara thelathini na tatu. Haya ni bora kwako kuliko mtumishi". [Imekubaliwa na Bukhari na Muslim. 6318-6915]

٣- قراءة سورة الإخلاص ، والمعوذتين قبل النوم : عن عائشة رضي الله عنها ، أن النبي - ﷺ . كان إذا أوى إلى فراشه كل ليلة جمع كفيه ثم نفث فيهما ، فقرأ فيهما : « قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ » و « قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ الْفَلَقِ » و « قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ » ، ثم يمسح بهما ما استطاع من جسده ، يبدأ بهما على رأسه ووجهه ، وما أقبل من جسده ، يفعل ذلك ثلاث مرات . [رواه البخاري : ٥٠١٧]

3- Kusoma Surat Al-Ikhlas na Al-

Mu'awwidhatayn [Qul A'audhu birabbi nnasi na Qul A'audhu birabbi Al Falaq] kabla ya kulala: Inapokewa kutoka kwa Aisha- Mwenyezi Mungu awe radhi naye- kwamba Mtume -Rehema na Amani za Allah zimfikie – “Alikuwa kila anapolala usiku, anakusanya mikono yake na kisha anapuliza ndani yake. Na husomea [Qul huwa llahu ahad] [Qul A'audhu birabbi nnasi] [Qul A'audhu birabbi Al Falaq] kisha anapangusa nayo sehemu ya mwili wake. awezavyo, akianzia juu ya kichwa na uso wake, na sehemu zinazofuata katika mwili wake, hufanya hivyo mara tatu. [Imepokewa na Al-Bukhari: 5017]

٤- الدّعاء حين الاستيقاظ أثناء النّوم: عن عبادة بن الصامت رضي الله عنه، عن النبي صلوات الله عليه وآله وسلامه. قال: ((من تعارَّ من الليل فقال: لا إله إلا الله وحده لا شريك له، له الملك وله الحمد، وهو على كل شيء قدير، الحمد لله، وسبحان الله ، والله أكبر، ولا حول ولا قوّة إلا بالله ، ثم قال: اللهم اغفر لي ، أو دعا ،استُجيب له ، فإنْ توضأ وصلَّى قُبْلَت صلاتِه)) [رواه البخاري: ١١٥٤]

4-Dua wakati wa kuamka kati kati ya usingizi:

Imepokewa na Ubada Ibn Al-Samit - Allah Amridhie- kutoka kwa Mtume - Rehema na Amani za Allah zimfikie - amesema: "Mwenye kuamka usiku na kusema: لا إله إلا الله وحده لا شريك له Hapana mungu apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah, peke yake ambaye hana mshirika, له الملك وله الحمد ufalme ni wake, na وهو على كل شيء قدير na Yeye ni Mwenye uweza juu ya kila kitu, الحمد لله sifa njema ni zake". سُبْحَانَ اللَّهِ Allah ametakasika na kila mapungufu, ، وَاللَّهُ أَكْبَرَ Allah ni mkubwa zaidi ، ولا حول ولا قوة إلا بالله Hakuna nguvu wala hila ila kwa Mwenyezi Mungu. Kisha akasema: Ewe Mola nisamehe, au akiomba, nitamkubalia, na akitawadha na akaswali, itakubaliwa swala yake" [Bukhari: 1154].

٥ - الدعاء عند الاستيقاظ من النوم بالدعاء الوارد : ((الحمد لله الذي أحياناً بعدهما أماتنا ، وإليه النشور)) [رواه البخاري من حديث حذيفة بن اليمان ﷺ: ٦٣١٢]

5- Dua ya kuamka usingizini, imethibiti

Dua hii:

“Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai baada ya kutufisha na kwake ni kufufuliwa”

[Bukhari ameipokea Hadithi ya Hudhaifah bin Al-Yaman – Allah amridhie: 6312]

SUNNAH ZA UDHU NA SALA

٦- المضمضة والاستنشاق من غرفة واحدة: عن عبدالله بن زيد رضي الله عنه ، أنَّ رسول الله صلوات الله عليه وآله وسلامه: ((تمضمض ، واستنشق من كف واحدة)) [رواه مسلم: ٥٥٥]

6- Kusukutua na na kutia maji puanī, kwa mchoto mmoja wa maji:

Kutoka kwa Abdullah bin Zaid Allah amridhie-, kwamba Mtume wa Allah - Rehema na Amani za Allah zimfikie- "Alisukutua kinywa chake na akatia maji puanī kwa mchoto mmoja (kwa mkono)" [Imepokewa na Muslim: 555]

٧-الوضوء قبل الفصل : عن عائشة رضي الله عنها ، أنَّ النبي صلوات الله عليه وآله وسلامه : ((كان إذا اغتسل من الجنابة، بدأ فغسل يديه، ثم توضأ كما يتوضأ للصلوة، ثم يدخل أصابعه في الماء، فيخلل بها أصول الشعر، ثم يصب على رأسه ثلات غُرف بيديه، ثم يُفيض الماء على جلده كله)) [رواه البخاري: ٢٤٨]

7- Kutawadha kabla ya kuoga:

Kutoka kwa Aisha -Allah amuwiye radhi- kwamba Mtume- Rehema na amani ya Allah zimfikie-: "Alikuwa anapo oga kutokana na Janaba, huanza kwa kuosha mikono yake, kisha anatawadha

kama anavyotawadha kwa ajili ya swala, kisha hutia vidole vyake ndani ya maji, na kuviingiza ndani ya nywele zake, kisha humiminia maji kichwani michoto mitatu, kisha huosha kwa maji mwili wake wote” [Al-Bukhari: 248]

٨-التشهد بعد الوضوء: عن عمر بن الخطاب - رضي الله عنه . قال: قال رسول الله ﷺ: ((ما منكم من أحد يتوضأ فيسبغ الوضوء ثم يقول: أشهد أنَّ لا إله إلا الله، وأنَّ محمداً عبده ورسوله إلاَّ فتحت له أبواب الجنة الشهانية، يدخل من أيها شاء)) [رواه مسلم: ٥٥٣]

8- Tashahhud (Dua) baada ya kutawadha:

Kutoka kwa Omar Ibn Al-Khattab –Allah amuwie radhi - amesema: Mtume wa Allah-Rehema na Amani za Allah zimfikie- amesema: “Hatawadhi mionganini mwenu na kutawadha vizuri kisha akasema: Nashuhudia ya kwamba hapana mungu apasae kuabudiwa kwa haki ila Allah, na kwamba Muhammad ni mja wake na Mtume wake isipokuwa itafunguliwa milango minane ya Pepo, ataingia autakao) [Imepokewa na Muslim: 553]

٩- الاقتصاد في الماء: عن أنس - رضي الله عنه . قال: ((كان النبي - ﷺ - يغسل بالصاع إلى خمسة أمداد ، ويتوضاً بالمُد)) [متفق عليه: ٢٠١ - ٧٣٧]

9- Kuhifadhi maji kwa kutumia kwa wastani:

Kutoka kwa Anas -Allah amridhie- amesema: "Mtume -Rehema na Amani zimfikie- alikuwa akioga kiasi cha Sa'a mpaka Mud tano, na kutawadha kwa Mud moja" [Imekubaliwa: 201-737]

- Sa'a: ni kipimo cha ujazo wa Mud nne.
- Mud: ni kipimo cha ujazo wa kiasi cha kuja mikono miwili ikikusanywa pamoja.

١٠ - صلاة ركعتين بعد الوضوء: قال النبي ﷺ: ((من توضأ نحو وضوئي هذا، ثم صلى ركعتين لا يحذثُ فيها نفسه ، غُفر له ما تقدم من ذنبه)) [متفق عليه من حديث حُرمان مولى عثمان رضي الله عنهما: ١٥٩ - ٥٣٩]

10- Kuswali rakaa mbili baada ya kutawadha:

Mtume – Rehema na Amani za Allah zimfikie - kasema: "Mwenye kutawadha namna hivi ninavyo tawadha, kisha akaswali rakaa mbili bila ya kuizungumzisha nafsi yake (maneno ya nje ya swala), atasamehewa madhambi yake

yaliyotangulia” [wameafikiana Bukari na Muslim, katika Hadithi ya Humran. Mtumwa Uthman, Mungu awe radhi nao: 159-539]

١١ - التَّرْدِيدُ مَعَ الْمُؤْذِنِ، ثُمَّ الصَّلَاةُ عَلَى النَّبِيِّ ﷺ: عن عبد الله بن عمرو رضي الله عنهما ، أنه سمع النبي - ﷺ . يقول: ((إِذَا سَمِعْتَ الْمُؤْذِنَ فَقُولُوا مِثْلَ مَا يَقُولُ، ثُمَّ صَلُوْا عَلَيْهِ ، فَإِنَّهُ مِنْ صَلَّى عَلَيْهِ صَلَاةً ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ بِهَا عَشْرًا ... الْحَدِيثُ)) [رواه مسلم: ٨٤٩]

11- Kurudia maneno ya Muadhini, kisha kumswalia Mtume –Rehema na Amaani zimfikie-:

Kutoka kwa Abdullah bin Amr -Mwenyezi Mungu awe radhi nao- kwamba alimsikia Mtume –Rehema na Amani za Allah zimfikie-akisema: “Mkisikia Muadhini basi semeni sawa na asemavyo, na niswalieni, hakika atakaeniswalia mimi mara moja, Allah atamrehemu mara kumi.... Hadithi.” [Imepokewa na Muslim: 849].

ثم يقول بعد الصلاة على النبي ﷺ: (اللهم رب هذه الدعوة التامة ، والصلوة القائمة ، آتِ محمداً الوسيلة والفضيلة ، وابعثه مقاماً حموداً الذي وعدته) [رواه البخاري. من قال ذلك حلت له شفاعة النبي ﷺ]

Kisha anasema baada ya kumswalia Mtume – Rehema na Amani ziwe juu yake-: “Ewe Mola Mlezi wa wito huu mkamilifu na sala iliyosimama, mpe Muhammad njia na wema, na umnyanyue kwenye daraja tukufu ulilomuahidi” [Imepokewa na Bukhari. Mwenye kusema hivyo, atapata uombezi wa Mtume]

١٢ - الإِكْثَارُ مِنِ السُّوَاكِ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: (لَوْلَا أَنْ أُشْقَى عَلَى أُمَّتِي، لَأُمْرِتُهُمْ بِالسُّوَاكِ عِنْدَ كُلِّ صَلَاةٍ) [متفق علىه: ٥٨٩ - ٨٨٧].

12- Kupiga mswaki mara kwa mara:

Kutoka kwa Abu Hurairah –Allah amridhie-kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu –Rehema na Amani za Allah zimfikie- amesema: “Lau isingekuwa kuwapa uzito umma wangu, ningewaamrishwa kutumia mswaki, katika kila Swala.” [Imekubaliwa na Bukhari na Muslim: 887-589].

** Pia ni katika Sunnah kutumia mswaki wakati wa kuamka kutoka usingizini, wakati wa kutawadha, na wakati harufu ya mdomo inabadilika, na wakati wa kusoma Qur'an, na wakati wa kuingia nyumbani.

١٣- التبكيـر إلـى المسـجد : عن أبي هـرـيـرة - رـضـيـ اللـهـ عـنـهـ . قال: قال رسول الله ﷺ: ((... ولو يـعـلـمـونـ مـاـ فـيـ التـهـجـيرـ [التبـكـيرـ] لـاستـقـواـ إـلـيـهـ ... الحـدـيـثـ)) [مـتفـقـ عـلـيـهـ: ٦١٥ - ٩٨١].

13- Kuelekea msikitini mapema:

Kutoka kwa Abu Hurairah –Allah amridhie-amesema: Mtume wa Allah –Rehema na Amani za Allah zimfikie- amesema: "Lau watu wangejua (ubora) wa kuwahi mapema (kwenda kuswali), wangeshindana kwa hilo..." Hadithi" [Imekubaliwa na Bukhari na Muslim: 615-981].

١٤- الذهـاب إلـى المسـجد ماـشـياً : عن أبي هـرـيـرة - رـضـيـ اللـهـ عـنـهـ ، أن رسول الله ﷺ . قال: ((أـلـاـ أـدـلـكـمـ عـلـىـ مـاـ يـمـحـوـ اللـهـ بـهـ الـخـطـاـيـاـ ، وـيـرـفـعـ بـهـ الـدـرـجـاتـ)) قـالـوـاـ: بـلـ يـاـ رـسـوـلـ اللـهـ . قـالـ: ((إـسـبـاغـ الـوـضـوـءـ عـلـىـ الـمـكـارـهـ ، وـكـثـرـةـ الـخـطـاـءـ إـلـىـ الـمـسـاجـدـ ، وـانتـظـارـ الـصـلـاـةـ بـعـدـ الـصـلـاـةـ ، فـذـلـكـمـ الرـبـاطـ)) [رواه مسلم: ٥٨٧].

14- Kwenda msikitini kwa miguu:

Kutoka kwa Abu Huraira –Allah amridhie-kwamba Mtume wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake- alisema: "Je, nisiwaambie jambo ambalo kwalo Mwenyezi Mungu anafuta

madhambi na kunyanya daraja? Wakasema: Twambie ewe Mtume wa Allah. Akasema: "Kutawadha wakati mgumu, kuchukua hatua nyingi kwenda Misikitini, na kungojea Swalah baada ya Sala, hiyo ni Ribat". [Imepokewa na Muslim: 587].
 Ribat: ni kujizuia katika kusubiri kufanya jambo la kheri.

١٥ - **إتيان الصلاة بسكينة ووقار:** عن أبي هريرة -رضي الله عنه- قال: سمعت رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَهُ وَبَرَّاهُ- يقول: ((إِذَا أَقِيمَتِ الصَّلَاةُ فَلَا تَأْتُوهَا تَسْعُونَ، وَأَتُوهَا تَمْشُونَ، وَعَلَيْكُمُ السَّكِينَةُ، فَمَا أَدْرَكْتُمْ فَصَلَوَا، وَمَا فَاتَكُمْ فَأَنْتُوا)) [متفق عليه: ٩٠٨ - ١٣٥٩]

15- Kuswali kwa utulivu na taadhima:

Kutoka kwa Abu Hurairah –Allah amridhie-amesema: Nimemsikia Mtume wa Allah – Rehemaa na Amani ya Allah zimfikie- akisema: "Ikianza Swalah msiiendee mbio, na njooni humo kwa kutembea, na muwe watulivu. Basi mnachokiwahi (katika swala) kitekelezeni, na mnachokikosa, kikamilisheni"

[Inakubaliwa na Bukhari na Muslim: 908 - 1359]

١٦ - الدعاء عند دخول المسجد، والخروج منه : عن أبي حميد الساعدي، أو عن أبي أُسَيْدٍ رضي الله عنها . قال: قال رسول الله ﷺ: ((إِذَا دَخَلْتُمُ الْمَسْجِدَ فَلْيَقُلْ: اللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ، وَإِذَا خَرَجْتُ فَلْيَقُلْ: اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ مِنْ فَضْلِكَ)) [رواه مسلم: ١٦٥٢].

16- Dua ya kuingia na kutoka msikitini:

Kutoka kwa Abu Humaid Al-Saadi, au kwa Abu Usayd –Allah awawie radhi wote wawili–amesema: Mtume wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: “mmoja wenu akiingia msikitini, na aseme: Ewe Mola nifungulie milango ya rehema yako, na anapotoka aseme: Ewe Mola wangu nakuomba fadhila zako” [Imepokewa na Muslim: 1652].

١٧ - الصلاة إلى ستة : عن موسى بن طلحة عن أبيه قال: قال رسول الله ﷺ: ((إِذَا وَضَعَ أَحَدُكُمْ بَيْنَ يَدِيهِ مِثْلَ مَؤْخِرَةِ الرَّحْلِ فَلْيُصَلِّ، وَلَا يَبَالْ مَنْ مَرَرَاءَ ذَلِكَ)) [رواه مسلم: ١١١١].

17- Kuswali hali ya kuweka mbele Sutrah (kinga):

Kutoka kwa Musa bin Talha, kutoka kwa baba yake, amesema: Amesema Mtume wa Allah –

Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake:- atakapo weka mmoja wenu mbele yake mfano wa kiegemeo cha mnyama, basi na aswali wala asijali kitakacho pita mbele yake”. [Amepokea Muslim: 1111].

SUTRAH:

Ni ile anayo iweka anae swalii mbele yake wakati wa kuswali, ili imkinge na kinachopita mbele yake, kisije kuharibu swala yake, kama vile ukuta, nguzo, inatakiwa iwe karibu theluthi mbili ya urefu wa mkono. Na imelinganishwa na kiegemeo cha mnyama kile ambacho huwa juu ya mnyama kama ngamia, na mtu huegemea wakati akiwa amempanda.

١٨- **الإِقْعَادُ بَيْنِ السَّجْدَتَيْنِ**: عن أبي الزَّيْرِ أَنَّهُ سَمِعَ طَاوُوسًا يَقُولُ:
 قلنا لابن عباس -رضي الله عنهما- في الإِقْعَادِ عَلَى الْقَدْمَيْنِ ، فَقَالَ : «هِيَ السُّنْنَةُ»
 فقلنا له: إننا لنراه جفاء بالرجل ، فقال ابن عباس: ((بل هي سُنْنَةُ نَبِيِّكَ
 . [رواه مسلم: ١١٩٨] وَبِحَمْدِ اللَّهِ))

18- Kukaa kikazi cha Al-Iqaa , (kukalia miguu miwili) kati ya Sijda mbili:

Kutoka kwa Abu Al-Zubayr kwamba alimsikia Twawuusi akisema: Tulimwambia Ibn Abbas – Allah amridhie- kuhusu Al-Iqaa, akasema: “Hiyo ni Sunnah”.

Tukamwambia: sisi tunalionna ni ishara ya ukavu wa mtu, akasema Ibn Abas – Allah amuwie Radhi- bali hiyo ni sunnah Ya Mtume wako ﷺ [Imepokewa na Muslim: 1198].

Al-Iqaa` ni: kunyoosha miguu na kukaa juu ya visigino, na huwa kati ya sijda mbili.

١٩ - التورك في التشهد الثاني: عن أبي حميد الساعدي - رضي الله عنه . قال: ((كان رسول الله ﷺ - إذا جلس في الركعة الآخرة ، قدم رجله اليسرى ، ونصب الأخرى ، وقعد على مقعده)) [رواه البخاري: ٨٢٨] .

19- Kukaa kikazi cha (Al-Tawwaruku) katika Tashahhud ya pili:

Kutoka kwa Abu Hamid al-Saadi –Allah amridhie- amesema: "Wakati Mtume wa Allah – Rehemaa na Amani za Allah zimfikie- akikaa katika rakaa ya mwisho, alikuwa akiulaza mguu wake wa kushoto, na kunyanya. mwingine, na hukaa kwa makalio yake." [Bukhari: 828].

٢٠ - الإكثار من الدعاء قبل التسليم: عن عبد الله بن عمر - رضي الله عنهما . قال: (كنا إذا كنا مع النبي ﷺ ... إلى أن قال: (ثم ليتخيير من الدعاء أعجبه إليه فيدعوه) [رواه البخاري: ٨٣٥] .

20- Kuomba dua nyingi kabla ya kutoa salam:

Kutoka kwa Abdullah bin Umar –Allah amuwiye radhi– amesema: "Tulikuwa tukiwa pamoja na Mtume ... Mpaka akasema: "Achague mmoja wenu dua anayoipenda basi na aiombe" [Bukhari: 835].

٢١- أداء السنن الرواتب: عن أم حبيبة رضي الله عنها، أنها سمعت رسول الله - ﷺ - يقول: ((ما من عبد مسلم يصلِّي الله كل يوم ثنتي عشرة ركعة طوعًا غير الفريضة ، إلا بني الله له بيًّا في الجنة)) [رواه مسلم: ١٦٩٦].

21- Kutekeleza Sunnah za kawaida (kabla na baada ya swala):

Kutoka kwa Ummu Habeeba -Allah amuwiye radhi- kwamba alimsikia Mtume wa Allah – Rehemaa na Amani za Allah ziwe juu yake-akisema: "Hakuna mja Mwislamu anayeswali rakaa kumi na mbili zisizo za Lazima (faradhi) ila Allah humjengea nyumba Peponi" [Muslim: 1696].

* Sunnah za kawaida: idadi yake ni Rakaa kumi na mbili, mchana na usiku: rakaa nne kabla ya adhuhuri, mbili baada ya adhuhuri, mbili baada

ya Maghribi, mbili baada ya Isha, na mbili kabla ya alfajiri.

٢٢ - صلاة الضحى: عن أبي ذر رضي الله عنه، عن النبي صلوات الله عليه وآله وسلامه. أنه قال: ((يصبح على كل سلامي (أي: مفصل) من أحدكم صدقة ، فكل تسبحة صدقة، وكل تهليلة صدقة، وكل تكبيرة صدقة، وأمر بالمعروف صدقة ، ونهي عن المنكر صدقة ، ويجزىء من ذلك ركعتان يركعهما من الضحى)) [رواه مسلم: ١٦٧١].

22- Swala ya Dhuha:

Kutoka kwa Abu Dhari –Allah amridhie- kutoka kwa Mtume –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kwamba amesema: "Inakuwa juu ya kila kiungo cha mmoja wenu Sadaka, basi kila tasbihi ni sadaka, kila kuhimidi ni sadaka, kila Tahlilah ni sadaka, na kila takbira ni sadaka, na kila amri ya kutenda mema ni sadaka, na kukataza maovu ni sadaka, na rakaa mbili za swala inayatosheleza yote swalah ya Dhuha"

[Muslim: 1671].

* Wakati ulio bora wa kuitekeleza ni wakati wa mchana, na jua ni kali sana, na mwisho wa wakati wake ni kuingia adhuhuri, na uchache

wake ni rakaa mbili, na hakuna mwisho wa wingi wake .

٢٣- **قيام الليل** : عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أن رسول الله صلوات الله عليه وآله وسلامه سُئل : أي الصلاة أفضل بعد المكتوبة ، فقال : «أفضل الصلاة بعد الصلاة المكتوبة ، الصلاة في جوف الليل » [رواه مسلم: ٢٧٥٦] .

23- Qiyaam al-Layl (swala ya usiku):

Kutoka kwa Abu Hurairah –Allah amridhie-Hakika Mtume aliulizwa: Ni Swala gani iliyo bora baada ya Swalah ya faradhi, akasema: Swala (inayoswaliwa) kati kati ya usiku” [Imepokewa na Muslim: 2756].

٤- **صلاة الوتر** : عن ابن عمر رضي الله عنهمَا ، أَنَّ النَّبِيَّ صلوات الله عليه وآله وسلامه - قال: «اجعلوا آخر صلاتكم بالليل وترًا» [منافق عليه: ٩٩٨ - ١٧٥٥] .

24- Swalah ya Witr:

Imepokewa na Ibn Umar, -Allah awawie radhi-kwamba Mtume –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: “Fanyeni swalah zenu za mwisho za usiku ni Witr”. [Imekubaliwa: 998 - 1755].

٢٥ - أداء صلاة النافلة في البيت : عن جابر - رضي الله عنه . قال: قال رسول الله صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((إذا قضى أحدكم الصلاة في مسجده ، فليجعل بيته نصيباً من صلاته، فإن الله جاعل في بيته من صلاته خيراً)) [رواه مسلم: ١٨٢٢].

25- Kuswali swala za Sunna nyumbani:

Imepokewa na Jaber -Allah amridhie-Amesema: Amesema Mtume wa Allah -Rehema na Amani za Allah zimfikie- "Akimaliza mmoja wenu Swala katika msikiti wake, basi na aifanye nyumba yake kuwa sehemu ya Swala yake, kwani Mwenyezi Mungu atamletea kheri nyumbani kwake kwa sababu ya swala yake". [Imepokewa na Muslim: 1822]

٢٦ - الصلاة في النعلين إذا تحققت طهارتها : سُئل أنس بن مالك رضي الله عنه: أكان النبي - صلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ . يصلي في نعليه؟ قال: (نعم) . [رواه البخاري: ٣٨٦].

26- Kuswali na viatu vikiwa visafi:

Aliulizwa Anas bin Malik: Je, Mtume, -Amani ziwe juu yake- aliswali hali ya kuwa amevaa viatu? Akasema: (Ndiyo). [Imepokewa na Al-Bukhari: 386].

٢٧ - **الصلوة في مسجد قباء:** عن ابن عمر - رضي الله عنهما . قال: (كان النبي - ﷺ - يأتي قباء راكباً و ماشياً) زاد ابن نمير: حدثنا عبيد الله، عن نافع: (فيصل في ركعتين). [متفق عليه: ١١٩٤ - ٣٣٩٠].

27- Kuswali katika Msikiti wa Qubaa:

Kutoka kwa Ibn Umar -Allah awawie radhi-amesema: "Mtume alikuwa akija Qubaa akiwa amepanda au anatembea". Ibn Numayr ameongeza, kutoka kwa Naafii: "Basi huswali Rakaa mbili ndani yake". [Inakubaliwa na Bukhari na Muslim: 1194-3390].

٢٨ - **الجلوس في المصلى بعد صلاة الفجر حتى تطلع الشمس:** عن جابر بن سمرة رضي الله عنه: (أن النبي - ﷺ - كان إذا صلى الفجر جلس في مصلاه حتى تطلع الشمس حسناً). [رواه مسلم: ١٥٢٦].

28- Kukaa sehemu ya kuswali baada ya Swalah ya alfajiri mpaka jua linapochomoza:

Imepokewa kutoka kwa Jabir bin Samra -Allah amridhie- : kwamba Mtume -Rehema na Amani ziwe juu yake- akiswali Alfajiri, alikuwa akikaa katika sehemu yake aliyo swalia mpaka jua lichomoze vizuri" [Imepokewa na Muslim: 1526].

٢٩- **الاغتسال يوم الجمعة :** عن ابن عمر - رضي الله عنهم - قال: قال رسول الله ﷺ: ((إذا جاء أحدكم الجمعة فليغتسل)) [متفق عليه: ٨٧٧ - ١٩٥١]

29- Kuoga siku ya Ijumaa:

Imepokewa kutoka kwa Ibn Umar –Allah amuwiye radhi- amesema: Mtume wa Allah amesema: "Aanapotaka kuja mmoja wenu kwenye Swalah ya Ijumaa basi na aoge" [Imekubaliwa kwa: 877-1951].

٣٠- **التبكير إلى صلاة الجمعة :** عن أبي هريرة - . قال: قال رسول الله ﷺ: ((إذا كان يوم الجمعة ، وقف الملائكة على باب المسجد ، يكتبون الأول فالأول ، ومثل المُهَجِّر (أي: المبكر) كمثل الذي يهدي بدنة ، ثم كالذي يهدي بقرة ، ثم كبشًا ، ثم دجاجة ، ثم بيضة ، فإذا خرج الإمام طروا صحفهم ، ويستمعون الذكر)) [متفق عليه: ٩٢٩ - ١٩٦٤] .

30- Kwenda mapema kwenye Swalah ya Ijumaa:

Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah –Allah amridhie- amesema: Mtume wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: "Ikifika siku ya Ijumaa، Malaika husimama mlangoni mwa

msikiti wakiandika wa kwanza kisha anaefutia na anaefuatia. Na mfano wa malipo ya alie wahi mapema ni kama ya kutoa Ngamia (sadaka), kisha (anaemfuatia) kama malipo ya Ng'ombe, kisha kama kondoo dume, kisha kuku, kisha yai, na imamu anapofika, wanakunja majalada yao, na wanasikiliza mawaidha (hotuba)" [Imekubaliwa na Bukhari na Muslim: 929 - 1964].

٣١- تحرى ساعة الإجابة يوم الجمعة: عن أبي هريرة رضي الله عنه، أن رسول الله صلوات الله عليه وآله وسلامه - ذكر يوم الجمعة فقال: ((فيه ساعة، لا يوافقها عبد مسلم، وهو قائم يصلي، يسأل الله تعالى شيئاً، إلا أعطاه إياه)) وأشار بيده يقللها. [منفق عليه: ٩٣٥ - ١٩٦٩].

31- Kutafuta muda wa kujibiwa dua siku ya Ijumaa:

Kutoka kwa Abu Huraira –Allah amridhie-kwamba Mtume wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alii taja siku ya Ijumaa na akasema: "Ndani yake kuna saa moja, na mja Mwislamu hatosadifiana nayo hali ya kuwa amesimama anaswali, anamuomba Allah Mtukufu, ila Allah humpa alicho kiomba" Na

akatoa ishara kwa mkono wake na kuonesha kuwa ni muda mchahe.

[Inakubaliwa na Bukhari na Muslim: 935 - 1969].

٣٢-الذهاب إلى مصلى العيد من طريق، والعودة من طريق آخر: عن جابر -رضي الله عنه- قال: ((كان النبي -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ -إِذَا كَانَ يَوْمُ عِيدٍ خَالِفَ الطَّرِيقَ))
[رواه البخاري: ٩٨٦].

32- Kwenda kwenye swala ya Idi kwa njia moja, na kurejea kwa njia nyingine:

Kutoka kwa Jabir –Allah amridhie- amesema: “Mtume –Rehema na Amani ziwe juu yake- ikiwa ni siku ya Idi, anabadilisha njia, (hupita njia tofauto na aliyojia)” [Bukhari: 986].

٣٣- الصلاة على الجنازة: عن أبي هريرة -رضي الله عنه- قال: قال رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ : ((من شهد الجنازة حتى يصلى عليها فله قيراط ، ومن شهدها حتى تدفن فله قيراطان)) قيل: وما القيراطان؟ قال: ((مثل الجبلين العظيمين)) [رواه مسلم: ٢١٨٩].

33- Swala ya Maiti:

Kutoka kwa Abu Huraira – Allah amridhie- amesema: Mtume Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: “Atakaye

hudhuria mazishi mpaka akaswali (Swala ya maiti) basi atapata Qiraati moja, na atakaye hudhuria mpaka azikwe basi atapata Qiraati mbili, Ikasemwa: Na Qiraati mbili ni nini? Akasema: Kama milima miwili mikubwa (malipo makubwa” [Imepokewa na Muslim: 2189].

* Kama milima miwili mikubwa: Anakusudia malipo makubwa.

٤- زيارة المقابر: عن بريدة -رضي الله عنه- قال: قال رسول الله صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: «كنت نهيتكم عن زيارة القبور فزوروها... الحديث» [رواه مسلم: ٢٢٦٠].

34- Kuzuru makaburi:

Inapokewa kutoka kwa Buraydah –Allah amridhie- amesema: Mtume wa Allah –Rehemha na Amani za Allah zimfikie- amesema: “Nilikuwa nikiwakataza kuzuru makaburi, basi yazuruni... Hadithi” [Muslim: 2260].

Tanbihi: Wanawake wamekatazwa kuzuru makaburi, kwani Sheikh Ibn Baz, Allah amrehemu, alitoa fatwa - ya kulikataza hilo - na pia kundi la wanazuoni.

٣٥ - صلاة الاستخاراة: عن جابر بن عبد الله . قال: (كان رسول الله . يعلّمنا الاستخاراة في الأمور كما يعلّمنا السورة من القرآن) . [رواه البخاري: ١١٦٢]

35- Swala ya Istikharah (kuomba kheri):

Imepokewa na Jaber bin Abdullah –Allah amridhie- Akasema: (Mtume wa Allah -Rehema na amani ziwe juu yake- alikuwa akitufundisha istikharah katika mambo kama anavyo tufundisha sura katika Qur’ani” [Bukhari: 1162].

** Na jinsi ya kuiswali ni kama ilivyo elezwa katika Hadithi iliyotangulia: kwamba mtu anaswali rakaa mbili, kisha anasema:

“Ewe Mwenyezi Mungu, mimi nakuomba muongozo unielekeze kwenye lililo la kheri, kwa ujuzi wako, na nakuomba uniwezeshe kwa uwezo wako, na nakuomba fadhila Zako kubwa, kwani Wewe ni muweza, na mimi siwezi, nawe Unajua nami sijui, na Wewe ndiye Mjuzi wa ghaibu, Ewe Allah kama wajua jambo hili (atalitaja jambo lenyewe) lina kheri na mimi katika dini yangu na maisha yangu na mwisho ya jambo langu, katika dunia yangu na Akhera yangu, basi nakuomba uniwezeshe kulipata, na unifanyie wepesi kisha unibariki humo, na ikiwa unajua ya kwamba jambo hili ni baya kwangu katika dini yangu, na maisha yangu, na mwisho wa mambo yangu, katika dunia yangu na Akhera yangu basi liepushe nami, nami niepushe nalo, na unipangie jambo lingine lenye kheri nami popote lilipo, kisha niridhishe nalo.”

SUNNA ZA KUFUNGA

٣٦- السحور: عن أنس -^{رضي الله عنه}- قال : قال رسول الله ^{صلوات الله عليه وآله وسلامه}: ((تسحروا؛ فإن في السحور بركة)) [متفق عليه: ١٩٢٣ - ٢٥٤٩] .

36- Kula Daku:

Kutoka kwa Anasi –Allah amridhie- amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "Kuleni Daku, hakika kwenye kula daku kuna Baraka". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 1923,2549]

٣٧-تعجيل الفطر ، وذلك إذا تحقق غروب الشمس : عن سهل بن سعد -^{رضي الله عنه}- قال: قال رسول الله ^{صلوات الله عليه وآله وسلامه}: ((لا يزال الناس بخير ما عجلوا الفطر)) [متفق عليه: ١٩٥٧ - ٢٥٥٤] .

37- Kuharakisha kufuturu, mara baada ya kuzama Jua:

Kutoka kwa Sahli Bin Saad –Allah amridhie- amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ya Allah ziwe juu yake- : "Watuhawatoacha kuwa katika kheri, muda wakuwa

wanaharakisha kufuturu". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 1957,2554]

٣٨- قيام رمضان : عن أبي هريرة رضي الله عنه، أن رسول الله صلوات الله عليه وآله وسلامه قال : ((من قام رمضان إيمانًا واحتسابًا غُفر له ما تقدم من ذنبه)) [متفق

عليه: ١٧٧٩-٣٧]

38- Swala ya usiku mwezi wa Ramadhani:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : "Mwenye kusimama (usiku wa) Ramadhani, kwa kumuamini Allah, na kutaraji malipo mema kwake, atasamehewa madhambi yake yaliyo tangulia". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 37,1779]

٣٩-الاعتكاف في رمضان، وخاصة في العشر الأواخر منه : عن ابن عمر رضي الله عنهما - قال: ((كان رسول الله صلوات الله عليه وآله وسلامه. يعتكف العشر الأواخر

من رمضان)) [رواه البخاري: ٢٠٢٥]

39- Kukaa Itikaaf katika mwezi wa Ramadhani, hasa kwenye kumi la mwisho:

Kutoka kwa Ibn Umar –Allah awaridhie-amesema: "Alikuwa Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akikaa Itikaf siku kumi za mwisho wa Ramadhani". [Amepokea Bukhary: 2025]

٤ - صوم ستة أيام من شوال: عن أبي أيوب الأنباري رضي الله عنه، أن رسول الله صلوات الله عليه وآله وسلامه قال: ((من صام رمضان ، ثم أتبعه ستًا من شوال ، كان كصيام الدهر)) [رواه مسلم: ٢٧٥٨]

40-Kufunga siku sita, mwezi wa Mfungo mosi:

Kutoka kwa Abuu Ayubu Al-answary –Allah amridhie- Hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: "Mwenye kufunga Ramadhani, kisha akaifatilizia kwa kufunga siku sita za mfungo mosi, atakuwa kama amefunga mwaka mzima". [Amepokea Muslim: 2758]

٤ - صوم ثلاثة أيام من كل شهر: عن أبي هريرة رضي الله عنه قال: ((أوصاني خليلي بثلاث ، لا أدعهن حتى الموت: صوم ثلاثة أيام من كل شهر، وصلاة الضحى ، ونوم على وتر)) [متفق عليه: ١١٧٨- ١٦٧٢]

41- Kufunga siku tatu kila mwezi:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-amesema: "Ameniusia kipenzi changu, mambo matatu, nisiaache mpaka kufa: Kufunga siku tatu kila mwezi, Swala ya Dhuhaa, na Kulala baada ya (swala) Witri". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 1178,1672]

٤٢ -صوم يوم عرفة: عن أبي قتادة رضي الله عنه، أن رسول الله صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قال: ((صيام يوم عرفة، أحتسب على الله أن يكفر السنة التي قبلة، والسنة التي بعده)) [رواه مسلم: ٣٧٤٦].

42-Kufunga siku ya Arafa:

Kutoka kwa Abuu Qatada –Allah amridhie-hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: "Funga ya siku ya Arafa, nataraji kwa Allah itafuta madhambi ya mwaka ulio pita na mwaka unao kuja". [Amepokea Muslim: 3746]

٤٣ - صوم يوم عاشوراء: عن أبي قتادة رضي الله عنه قال: قال رسول الله صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((صيام يوم عاشوراء ، أحتسب على الله أن يكفر السنة التي قبلة)) [رواه مسلم: ٣٧٤٦].

43- Kufunga siku ya Aashuraa:

Kutoka kwa Abuu Qatada –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : “Funga ya siku ya Aashuraa, nataraji kwa Allah itafuta madhambi ya mwaka ulio pita” [Amepokea Muslim: 3746]

SUNNA ZA SAFARI

٤ - اختيارات أمير في السفر: عن أبي سعيد، وأبي هريرة - رضي الله عنهما . قالا: قال رسول الله ﷺ: ((إذا خرج ثلاثة في سفر فليؤمروا أحدهم)) [رواه أبو داود: ٢٦٠٨] .

44- Kuchagua kiongozi mkiwa safarini:

Kutoka kwa Abuu Saiyd na Abuu Hurayra –Allah awaridhie- wamesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-: "Watakapo toka watatu (safarini), wamfanye kiongozi mmoja wao". [Amepokea Abuu Daud: 2608]

٥ - التكبير عند الصعود والتسبيح عند النزول: عن جابر -رضي الله عنه-. قال: ((كنا إذا صعدنا كبرنا، وإذا نزلنا سبحنا)) [رواه البخاري: ٢٩٩٤] .

45- Kusoma Takbira (Allahu akbar) wakati wa kupanda (mlima), na Tasbihi (Subhana Allah) wakati wa kushuka:

Kutoka kwa Jabir –Allah amridhie- amesema: "Tulikuwa tukipanda (mlima) tunasoma Takbira,

na tukiteremka tunasoma Tasbihi". [Amepokea Bukhary: 2994]

* Katika sunna ya safari: Kusoma Takbira wakati wa kupanda mlima na kusoma Tasbihi wakati wa mteremko.

٤٦ - الدعاء حين نزول منزل: عن خولة بنت حكيم - رضي الله عنها - قالت: سمعت رسول الله ﷺ يقول: ((من نزل منزلًا ثم قال: أعود بكلمات الله التامات من شر ما خلق ، لم يضره شيء ، حتى يرتحل من منزله ذلك)) [رواه مسلم: ٦٨٧٨].

46- Dua ukifika katika nyumba yeyote:

Kutoka kwa Khaula Bint Hakiim –Allah amridhie-amesema: nimemsikia Mjumbe wa Allah – Rehemaa na Amani ya Allah ziwe juu yake-akisema: "Mwenye kufika kwenye nyumba yoyote, kisha akasema: Najilinda kwa maneno ya Allah yaliyo timia, kutokana na shari ya alicho kiumba, hakito mdhuru chochote mpaka aondoke kwenye hiyo nyumba". [Amepokea Muslim: 6878]

٤٧ - الْبَدْءُ بِالسَّجْدَةِ إِذَا قَدِمَ مِنَ السَّفَرِ: عَنْ كَعْبِ بْنِ مَالِكٍ - رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ -
 قال: ((كان النبي - ﷺ - إذا قدم من سفر بدأ بالمسجد فصل فيه))
 [متفق عليه: ٤٤٣ - ١٦٥٩].

47- Kufikia Msikitini, akirudi kutoka safari:

Kutoka kwa Kaab Bin Maliki –Allah amridhie-amesema: "Alikuwa Nabii –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akirudi kutoka safari, huanza kupita Msikitini na akaswali (Sunna)". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim: 443,1659]

SUNNA ZA MAVAZI NA CHAKULA

- ٤٨ - **الدعاء عند لبس ثوب جديد:** عن أبي سعيد الخدري - رضي الله عنه - قال: كان رسول الله - صلى الله عليه وسلم - إذا استجد ثوباً سماه باسمه : إما قميصاً، أو عمامة، ثم يقول: ((اللهم لك الحمد، أنت كسوتني، أسألك من خيره ، وخير ما صنع له ، وأعوذ بك من شره ، وشر ما صنع له)) [رواه أبو داود: ٤٠٢٠].

48- Dua wakati wa kuvaan Nguo mpya:

Kutoka kwa Abuu Saiyd Al-khud-ry –Allah amridhie- amesema: Alikuwa Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-akipata nguo mpya, anaitaja kwa jina lake, kanzu ama kiremba, kisha anasema: "Ewe Mwenyezi Mungu, ni zako wewe tu sifa njema, wewe ndio uliye nivisha hii nguo, ninakuomba kheri yake na kheri ya kilicho tengenezewa, na ninajilinda kwako na shari yake na shari ya kilicho tengenezewa". [Amepokea Abuu Daud: 4020]

- ٤٩ - **لبس النعل باليمين :** عن أبي هريرة - رضي الله عنه - قال: قال رسول الله - صلى الله عليه وسلم -: ((إذا اتّعل أحدكم فليبدأ باليمني ، وإذا خلع فليبدأ

بالشمال، ولينعلهم جمِيعاً، أو ليخلعهم جمِيعاً)) [متفق عليه: ٥٨٥٥ - ٥٤٩٥].

49- Kuva viatu, kuanza mguu wa kulia:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake:- “Akivaa viatu mmoja wenu, na aanze mguu wake wa kulia, na atakapo vua aanze mguu wa kushoto, na (akitembea) ima avae vyote au avue vyote”. [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 5855,5495]

٥٠- **القسمية عند الأكل:** عن عمر بن أبي سلمة -رضي الله عنه-. قال: كنت في حجر رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ- وكانت يديه تطيش في الصحفة ، فقال لي: ((يا غلام سم الله ، وكل بيمنيك ، وكل مما يليك)) [متفق عليه: ٥٣٧٦ - ٥٢٦٩].

50- Kusoma Bismil-lahi wakati wa kula:

Kutoka kwa Umar Bin Abii Salama –Allah amridhie-amesema: Nilikuwa kwenye Malezi ya Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- Ukawa mkono wangu unaizunguka sahani (wakati wa kula), Akaniambia: Ewe kijana! Soma Bismillah,

kula kwa mkono wa kulia, na kula (chakula) kinacho kuelekea". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 5376,5269]

٥١ - حمد الله بعد الأكل والشرب: عن أنس بن مالك –رضي الله عنه– قال: قال رسول الله ﷺ: ((إِنَّ اللَّهَ لِي رُضِيَّ عَنِ الْعَبْدِ أَنْ يَأْكُلَ الْأَكْلَةَ فِي حِمْدَهِ عَلَيْهَا، أَوْ يَشْرَبَ الشَّرْبَةَ فِي حِمْدَهِ عَلَيْهَا)) [رواه مسلم: ٦٩٣٢].

51-Kumshukuru Allah baada ya kula na kunywa:

Kutoka kwa Anasi Bin Maliki –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : "Hakika Allah anamridhia mja wake akila mlo wowote ule akamshukuru kwa hilo, na akinywa kinywaji akamshukuru kwa hicho". [Amepokea Muslim: 6932]

٥٢ - الجلوس عند الشرب : عن أنس –رضي الله عنه–، عن النبي ﷺ : ((أَنَّهُ أَنْ يَشْرَبَ الرَّجُلُ قَائِمًا)) [رواه مسلم: ٥٢٧٥].

52- Kukaa wakati wa kunywa:

Kutoka kwa Anasi –Allah amridhie- kutoka kwa Nabii –Rehema na Amani za Allah ziwe juu

yake- : "Hakika Mtume amekataza mtu kunywa akiwa amesimama". [Amepokea Muslim: 5275]

٥٢- **الضمة من اللبن:** عن ابن عباس -رضي الله عنهما-، أن رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَهُ- شرب
لبنًا فمضمض، وقال: ((إن له دسمًا)) [متفق عليه: ٧٩٨ - ٥٦٩].

53- Kusukutua baada ya kunywa Maziwa:

Kutoka kwa Ibn Abasi -Allah amridhie- Hakika Mjumbe wa Allah, alikunywa Maziwa kisha akasukutua, na akasema: "Hakika maziwa yana mafuta". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 798,5609]

٤٤ - **عدم عيب الطعام:** عن أبي هريرة -رضي الله عنهما- قال: ((ما عاب رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَهُ-. طعامًا قط، كان إذا أشتهاه أكله، وإن كرهه تركه)) [متفق عليه: ٥٣٨٠ - ٥٤٠٩].

54- Kuto kukitia kasoro chakula:

Kutoka kwa Abuu Hurayra -Allah amridhie- amesema: "Hakukitia kasoro Mjumbe wa Allah chakula, alikuwa akikipenda anakila, na asipo kipenda anakiacha". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 5409,5380]

٥٥ - الاكل بثلاثة أصابع: عن كعب بن مال -رضي الله عنه- قال: ((كان رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلامه- يأكل بثلاث أصابع ، ويلعق يده قبل أن يمسحها)) [رواه مسلم: ٥٢٩٧]

55- Kula kwa (kutumia) vidole vitatu:

Kutoka kwa Kaab Bin Maliki –Allah amridhie-amesema: Alikuwa Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake- akila kwa vidole vitatu, na alikuwa anaramba mkono wake kabla ya kuufuta”. [Amepokea Muslim: 5297]

٥٦ - الشرب والاستشفاء من ماء زمزم: عن أبي ذر -رضي الله عنه- قال: ((رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلامه- عن ماء زمزم: ((إنها مباركة ، إنها طعام طعم)) [رواه مسلم: ٦٣٥٩] وزاد الطيالسي: ((وشفاء سقم)) .

56- Kunywa na kujitibu kwa Maji ya Zamzam:

Kutoka kwa Abuu Dharry –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- kuhusu maji ya zamzam: “Hayo ni maji yenye Baraka, hakika hayo ni chakula kinacho jitosheliza”. [Amepokea Muslim: 6359], ameongeza Al-twayalusy: “ni tiba ya maradhi”.

٥٧ - الاكل يوم عيد الفطر قبل الذهاب للمصلى: عن أنس بن مالك -
 ضعيفه . قال: ((كان رسول الله ﷺ لا يغدو يوم الفطر حتى يأكل
 تمرات)) وفي رواية: ((ويأكلهن وترًا)) [رواه البخاري: ٩٥٣]

57- Kula siku ya Eid Al-fitri kabla ya kwenda kuswali:

Kutoka kwa Anasi Bin Maliki –Allah amridhie-amesema: “Alikuwa Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- hatoki siku ya Eid mpaka ale Tende”. Na katika Riwaya nyingine: “Alikuwa akizila himzo (Tende) witri”. [Amepokea Bukhary: 953]

DHIKRI (KUMTAJA ALLAH) NA DUA

٥٨ - **الإكثار من قراءة القرآن** : عن أبي أمامة الباهلي -رضي الله عنه- قال: سمعت رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلامه- يقول: ((اقرؤوا القرآن ، فإنه يأتي يوم القيمة شفيعاً لأصحابه)) [رواه مسلم: ١٨٧٤].

58- Kusoma sana Qur-an:

Kutoka kwa Abuu Umama Al-baahily -Allah amridhie- amesema: nimemsikia Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akisema: "Isomeni sana Qur-an, hakika hiyo itakuja siku ya Kiyama ikiwa ni muombezi kwa aliye isoma". [Amepokea Muslim: 1874]

٥٩ - **تحسين الصوت بقراءة القرآن** : عن أبي هريرة -رضي الله عنه-، أنه سمع رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلامه- يقول: ((ما أَذِنَ اللَّهُ لِشَيْءٍ مَا أَذِنَ لَنِبِيِّ حَسْنَ الصَّوْتِ ، يَتَعَنَّ بِالْقُرْآنِ يُجَهِّرُ بِهِ)) [متفق عليه: ٥٠٢٤ - ١٨٤٧].

59- Kusoma Qur-an kwa sauti nzuri:

Kutoka kwa Abuu Hurayra -Allah amridhie- Hakika alimsikia Mtume –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akisema: "Hajatoa ruhusa

Allah kwa chochote, kama alivyo mruhusu Nabii kuisoma Qur-an kwa sauti nzuri, anaighani Qur-an akiwa anasoma kwa sauti”. [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 5024,1847]

٦٠ - ذكر الله على كل حال: عن عائشة - رضي الله عنها - قالت: ((كان رسول الله - ﷺ - يذكر الله على كل أحيانه)) [رواه مسلم: ٨٢٦].

60- Kumtaja Allah kwa kila hali:

Kutoka kwa Aisha -Allah amridhie- amesema: “Alikuwa Mjumbe wa Allah -Rehemma na Amani ziwe juu yake- akimtaja Allah katika nyakati zake zote”. [Amepokea Muslim: 726]

٦١ - التسبیح: عن جويرية رضي الله عنها ، أن رسول الله - ﷺ - خرج من عندها بُكْرَة حین صلی الصبح ، وهي في مسجدها ، ثم رجع بعد أَنْ أَصْحَى ، وهي جالسة ، فقال: ((ما زلتِ على الحال التي فارقتك عليها ؟)) قالت: نعم ، قال النبي - ﷺ : ((لقد قُلْتُ بعده أربعَ كَلِمَاتٍ ، ثلَاثَ مراتٍ ، لَوْزِنَتْ بِمَا قُلْتَ مُنْذَ الْيَوْمَ لَوْزِنَتْ هُنْ : سبَّحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ ، عَدَدُ خَلْقِهِ ، وَرَضَا نَفْسِهِ ، وَزِنَةٌ عَرْشِهِ ، وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ)) [رواه مسلم: ٢٧٢٦]

61- Kumsabihi Allah (Subhana Allah):

Kutoka kwa Juwayriya –Allah amridhie- Hakika Mtume wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alitoka kwake mapema, baada ya swala ya Al-fajiri, ilihali (Juwayriya) yupo kwenye mswala wake, kisha akarudi wakati wa Dhuhaa akamkuta palepale amekaa, akamuuliza: Bado upo kwenye hali niliyokuacha nayo? Akasema: ndio, Akasema Nabii –Rehema na Amani ziwe juu yake- : Hakika baada ya kuondoka hapa, nimetamka maneno manne kwa mara tatu, lau yakipimwa na maneno yako yote uliyo yasema leo, yangezidi uzito (yakwangu): Utakasifu ni wake Allah, na shukrani ni zake, kwa Idadi ya viumbe wake, na Ridhaa ya nafsi yake, na kwa uzito wa Arshi yake, na uwingi wa maneno yake”. [Amepokea Muslim: 2726]

٦٢ - **تشمیت العاطس:** عن أبي هريرة رضي الله عنه، عن النبي صلوات الله عليه وآله وسلامه. قال:
 ((إذا عطس أحدهم فليقل: الحمد لله ، وليرسل له أخوه أو صاحبه: يرحمك الله. فإذا قال له: يرحمك الله، فليقل: يهديكم الله ويعصيكم بالكم)) [رواه البخاري: ٦٢٢٤]

62- Kumuombea Dua aliye piga chafya:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-kutoka kwa Nabii –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: Atakapo piga chafya mmoja wenu, na aseme: "Alhamdulillah (Namshukuru Allah), na amjibu ndugu yake ama rafiki yake: Yarhamuka Allah (Allah akurehemu), akisha muambia Allah akurehemu, basi na amjibu: Yah-diykumu Allahu wayus-lih baalakum (Allah akuongozeni na awatengenezee mambo yenu)". [Amepokea Bukhary: 6224]

٦٢ - الدعاء للمريض: عن ابن عباس رضي الله عنهم، أن رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ- دخل على رجل يعوده ، فقال عَنْ أَبِيهِ عَبَّاسٍ: ((لا بأس طهور، إن شاء الله)) [رواه البخاري: ٥٦٦٢]

63- Dua ya kumuombea mgonjwa:

Kutoka kwa Ibn Abasi –Allah awawie radhi- Hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- aliingia kwa mtu mmoja (mgonjwa) akiwa ameenda kumuona, akasema: "Hakuna ubaya kwako (juu ya maradhi haya), Allah ajaalie maradhi haya yawe kitu cha kufuta Madhambi, akipenda Allah". [Amepokea Bukhary: 5662]

٦٤ - وضع اليَدِ عَلَى مَوْضِعِ الْأَلْمِ، مَعَ الدُّعَاءِ: عَنْ عُثْمَانَ بْنِ أَبِي الْعَاصِ
 ﷺ، أَنَّهُ شَكَا إِلَى رَسُولِ اللَّهِ ﷺ. وَجَعًا، يَجْدِهِ فِي جَسَدِهِ مُنْذَ أَسْلَمَ،
 فَقَالَ لَهُ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: ((ضَعِ يَدَكَ عَلَى الَّذِي يَأْلَمُ مِنْ جَسَدِكَ)
 وَقَالَ: بِاسْمِ اللَّهِ، ثَلَاثًا، وَقُلْ سَبْعَ مَرَاتٍ: أَعُوذُ بِاللَّهِ وَقُدْرَتِهِ مِنْ شَرِّ
 مَا أَجِدُ وَأَحَادِرُ)) [رواه مسلم: ٥٧٣٧]

64- Kuweka mkono sehemu yenyemamu na kuomba Dua:

Kutoka kwa Uthmani Bin Abii Al-aas –Allah amridhie- hakika yeye alishtakia kwa Mtume maumivu anayoyapata kwenye mwili wake tangu alipo silimu, Mtume –Rehema na Amani ziwe juu yake- alimuambia: "Weka mkono wako sehemu yenyemamu, kisha sema: Bismillah (kwa jina la Allah), mara tatu, na sema mara saba: Audhubillahi waqud-ratihi min sharri ma ajidu wauhaadhiru (Najilinda kwa Allah, na kwa uwezo wake, kutokana na shari ninayo ipata na ninayo tahadhari)". [Amepokea Muslim: 5737]

٦٥ - الدُّعَاءُ عَنْدَ سَمَاعِ صِيَاحِ الدِّيَكِ، وَالتَّعْوِذُ عَنْدَ سَمَاعِ نَهْيِقِ الْحَمَارِ:
 عَنْ أَبِي هَرِيرَةَ ﷺ، أَنَّ النَّبِيَّ ﷺ قَالَ: ((إِذَا سَمِعْتُمْ صِيَاحَ الدِّيَكِ

فاسأّلوا الله من فضله، فإنّها رأت ملّكاً، وإذا سمعتم ثنيق الحمار
فتغدو بالله من الشيطان، فإنّها رأت شيطاناً) [متفق عليه: ٦٩٢٠ - ٣٣٠٣].

65- Dua inayo ombwa kwa kusikia sauti ya Jogoo, kujilinda kwa Allah kwa kusikia sauti ya Punda:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-hakika Nabii –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: “Mkisikia sauti ya Jogoo ombeni Fadhila za Allah, kwani hua amewaona Malaika, na mkisikia sauti ya Punda, takeni Hifadhi kwa Allah kutokana na Shetani, kwani huyo amemuona Shetani”. [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 3303,6920]

٦٦- الدّعاء عند نزول المطر: عن عائشة رضي الله عنها ، أن
رسول الله ﷺ . كان إذا رأى المطر قال: ((اللّهُمَّ صَبِّرْنَا
[رواه البخاري: ١٠٣٢]

66- Dua wakati wa kunyesthesia mvua:

Kutoka kwa Aisha –Allah amridhie- Hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- alikuwa akiona Mvua husema:

“Ewe Allah! (Tunakuomba) mvua iwe yenye manufaa”. [Amepokea Bukhary: 1032]

٦٧ - ذكر الله عند دخول المنزل : عن جابر بن عبد الله -رضي الله عنهما-. قال : سمعت النبي -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ- يقول : ((إِذَا دَخَلَ الرَّجُلُ بَيْتَهُ فَذَكِرْ اللَّهَ -عَزَّ وَجَلَّ- عَنْ دَخْولِهِ ، وَعَنْدِ طَعَامِهِ، قَالَ الشَّيْطَانُ : لَا مَبْيَتٌ لَكُمْ وَلَا عَشَاءٌ . إِذَا دَخَلَ فَلَمْ يَذْكُرْ اللَّهَ عَنْ دَخْولِهِ ، قَالَ الشَّيْطَانُ : أَدْرَكْتُمُ الْمَبْيَتِ ، وَإِذَا لَمْ يَذْكُرْ اللَّهَ عَنْ طَعَامِهِ ، قَالَ : أَدْرَكْتُمُ الْمَبْيَتِ وَالْعَشَاءَ)) [رواه مسلم: ٥٢٦٢] .

67- Kumontaja Allah wakati wa kuingia nyumbani:

Kutoka kwa Jaabir Bin Abdillahi –Allah amridhie-amesema: Nimemsikia Nabii –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: “Atakapo ingia mtu nyumbani kwake, akamtaja Allah –Mtukufu-wakati wa kuingia na wakati wa kula, Husema Shetani (kuwaambia wenzie): Hakuna kambi kwenu wala chakula, na asipomtaja (Allah) wakati wa kuingia, Husema Shetani: Mmepata sehemu ya kulala, na asipomtaja wakati wa kula pia, Husema: Mmepata sehemu ya kulala na sehemu ya kula”. [Amepokea Muslim: 5262]

٦٨- ذكر الله في المجلس: عن أبي هريرة رضي الله عنه، عن النبي صلوات الله عليه قال: ((ما جلس قوم مجلساً لم يذكروا الله فيه ، ولم يُصلوا على نبيهم، إلا كان عليهم ترة (أي: حسرة) فإن شاء عذبهم، وإن شاء غفر لهم)) [رواه الترمذى: ٣٣٨٠].

68- Kumontaja Allah kwenye kikazi:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-kutoka kwa Nabii –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: "Hawajapata kukaa watu kikazi chochote kile, kisha hawakumtaja Allah, na wala hawakumswalia Mtume wao, isipokuwa watu hao wamepata hasara, akitaka (Allah) atawaadhibu na akitaka atawasamehe". [Amepokea Al-tirmidhy: 3380]

٦٩- الدعاء عند دخول الخلاء: عن أنس بن مالك رضي الله عنه. قال: كان النبي صلوات الله عليه إذا دخل (أي: أراد دخول) الخلاء قال: ((اللهم إني أعوذ بك من الخبر والخائث)) [متفق عليه: ٦٣٢٢ - ٨٣١].

69- Dua wakati wa kuingia chooni:

Kutoka kwa Anas Bin Maliki –Allah amridhie-amesema: Alikuwa Nabii –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akiingia (akitaka kuingia)

chooni, husema: "Allhumma inniy audhubika minal-khubuthi walkhabaaithi (Ewe Allah! Hakika ninajilinda kwako na Mashetani wakiume na wakike)". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 6322,831]

٧٠-الدُّعَاءُ عِنْدَمَا تَعَصَّفَ الْرِّيحُ: عن عائشة -رضي الله عنها- قالت: كان النبي -صلوات الله عليه وآله وسلامه- إذا عصفت الريح قال: ((اللهم إني أأسألك خيرها، وخير ما فيها، وخير ما أرسلت به، وأعوذ بك من شرها، وشر ما فيها، وشر ما أرسلت به)) [رواه مسلم: ٢٠٨٥]

70- Dua wakati wa kuvuma upemo mkali (kimbunga):

Kutoka kwa Aisha –Allah amridhie- amesema: Alikuwa Mtume, ukivuma upemo, anasema: "Ewe Allah, Hakika ninaomba heri zake, na heri zilizopo humo, na heri zilizotumwa humo, na nina jilinda kwako na shari zake, na shari zilizopo humo, na shari zilizotumwa humo". [Amepokea Muslim: 2085]

٧١- الدُّعَاءُ لِلْمُسْلِمِينَ بِظُهُورِ الْغَيْبِ: عن أبي الدرداء -رضي الله عنه-، أنه سمع رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلامه- يقول: ((من دعا لأنبيائه بظهور الغيب، قال الملك الموكّل به: آمين ، ولك بمثل)) [رواه مسلم: ٦٩٢٨].

71- Kuwaombea Dua waislam, kwa siri:

Kutoka kwa Abuu Dardai –Allah amridhie- yeye alimsikia Mtume –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- akisema: "Mwenye kumuombea ndugu yake kwa siri, wanasema Malaika walio wakilishwa kwake: Amin, nawewe ulipwe mfano wake". [Amepokea Muslim: 6928]

٧٢-**الدعا عند المضيبيه**: عن أم سلمة . رضي الله عنها . أنها قالت ، سمعت رسول الله - ﷺ - يقول : ((ما من مسلم تصيبه مصيبة فيقول ما أمره الله : إنا لله وإننا إليه راجعون ، اللهم أُجرني في مُصيبيتي وأَخْلِف لي خيراً منها . إلا أخلف الله له خيراً منها))

[رواه مسلم: ٢١٢٦]

72- Dua wakati wa matatizo:

Kutoka kwa Ummu Salama –Allah amridhie-hakika yeye amesema: Nimemsikia Mtume – Rehema na Amani ziwe juu yake- anasema: "Hakuna Muislam yejote aliye patwa na tatizo, kisha akayasema aliyo muamrisha Allah: Innaa lillahi wainnaa ilayhi raajiuun (Hakika sisi sote ni wa Allah, na hakika kwake tutarejea), Allahumma ajiniy fii muswibatiy waakhlif lii khayran min-haa (Ewe Allah nilipe kwenye

msiba wangu huu, na nipe badala iliyokuwa bora zaidi), Isipokuwa Allah atampa kilicho bora zaidi". [Amepokea Muslim: 2126]

٧٣-إفشاء السلام: عن البراء بن عازب -رضي الله عنه-. قال: ((أمرنا النبي -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ- بسبع ، ونهانا عن سبع: أمرنا بعيادة المريض، ... وإفشاء السلام،... الحديث)) [متفق عليه: ٥١٧٥ - ٥٣٨٨].

73- Kusalimiana:

Kutoka kwa Baraa'i Bin Aazib –Allah amridhie-amesema: "Ametuamrisha Mtume –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- mambo saba: Ametuamrisha kuwatembalea wagonjwa, ... na kutoleana Salaam, ...". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 5175,5388]

SUNNA MBALI MBALI

٧٤- طلب العلم: عن أبي هريرة -رضي الله عنه-. قال: قال رسول الله ﷺ: ((من سلك طريقاً يلتمس فيه علماً سهل الله له به طريقاً إلى الجنة)) . [رواه مسلم: ٦٨٥٣]

74- Kutafuta Elimu:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah -Rehema na Amani ziwe juu yake- "Mwenye kupita njia, akiwa anatafuta Elimu, Allah humpa wepesi njia ya kwenda peponi". [Amepokea Muslim: 6853]

٧٥- الاستئذان قبل الدخول ثلاثاً: عن أبي موسى الأشعري -رضي الله عنه-. قال: ((الاستئذان ثلاث، فإن أذن لك، وإن فارجع)) [منتقى عليه: ٥-٦٢٤٥ - ٥٦٣٣].

75- Kupiga hodi mara tatu, kabla ya kuingia:

Kutoka kwa Abuu Musa Al-ashary –Allah amridhie- Hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake amesema:

"Kupiga hodi ni mara tatu, ukiruhusiwa ingia, usipo ruhusiwa rudi". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 6245,5633]

٧٦ - **تحنيك المولود** : عن أبي موسى الأشعري -رضي الله عنه- . قال: ((ولد لي غلام ، فأتيت به النبي -صلوات الله عليه وآله وسلام- . فسماه إبراهيم ، فحنكه بتمرة ودعا له بالبركة ... الحديث)) [متفق عليه: ٥٤٦٧ - ٥٦١٥]

76- Kumrambisha mtoto mchanga kitu kitamu:

Kutoka kwa Abuu Musa Al-ashary –Allah amridhie-amesema: Nilipata mtoto, nikampeleka kwa Mtume –Rehemna Amani za Allah ziwe juu yake-Akamuita Ibrahim, akamrambisha tende, akamuombea baraka, ...". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 5467,5615]

* Kumrambisha kitu kitamu ni: Kukitafuna kitu kitam kisha kumrambisha mtoto mchanga, na tende ni bora zaidi.

٧٧ - **الحقيقة عن المولود** : عن عائشة - رضي الله عنها - . قالت : ((أمرنا رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلام- . أن نعق عن الجارية شاة ، وعن الغلام شاتين)) [رواه أحمد: ٢٥٧٦٤]

77- Kumfanyia Akika mtoto:

Kutoka kwa Aisha –Allah amridhie- amesema: "Ametuamrisha Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake- tumfanyie Akika mtoto wa kike (kwa kuchinja) mbuzi mmoja, na mtoto wa kiume mbuzi wawili". [Amepokea Ahmad: 25764]

٧٨- كشف بعض البدن ليصييه المطر: عن أنس -رضي الله عنه- قال: أصحابنا مع رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلامه- مطر . قال: فحسر رسول الله -صلوات الله عليه وآله وسلامه- عن ثوبه حتى أصحابه من المطر ، فقلنا: يا رسول الله! لم صنعت هذا؟ قال: لأنّه حديث عهد بربه)) [رواه مسلم: ٢٠٨٣]

78- Kufunua sehemu ya mwili ili ipatwe mvua:

Kutoka kwa Anasi –Allah amridhie- amesema: Tulinyeshewa Mvua tukiwa pamoja na Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani zimfikie- akasema: Aliweka wazi Mtume baadhi ya sehemu ya mwili wake, mpaka ikanyeshewa mvua, Tukasema: Ewe Mjumbe wa Allah! Kwa nini umefanya hivi? Akajibu: "Hakika hiyo (mvua), ni mpya kutoka kwa Mola wake mlezi". [Amepokea Muslim: 2083]

٧٩ - عيادة المريض: عن ثوبان ، مولى رسول الله ﷺ ، عن رسول الله ﷺ قال: «من عاد مريضا ، لم يزل في حُرفة الجنة» قيل : يا رسول الله ! وما حُرفة الجنة؟ قال: ((جناها)) [رواه مسلم: ٦٥٤] .

79- Kumtembelea mgonjwa:

Kutoka kwa Thauban Mtumwa wa Mtume – Rehemaa na Amani ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume, amesema: “Yeyote mwenye kumtembelea mgonjwa, hatoacha kuwa Khurfatal-janna (mwenye kuchuma matunda ya peponi), wakamuuliza nini maana ya Khurfatal-janna? Akasema: ni matunda ya peponi” [Amepokea Muslim: 6554]

٨٠ - التبسم: عن أبي ذر رضي الله عنه قال: قال لي النبي ﷺ: ((لا تحررن من المعروف شيئا ، ولو أن تلقى أخيك بوجه طلق)) [رواه مسلم: ٦٦٩٠] .

80-Kutabasamu:

Kutoka kwa Abuu Dhari –Allah amridhie-amesema: aliniambia Nbii –Rehemaa na Amani ya Allah ziwe juu yake- : “Usidharau chochote katika mema, japo kukutana na ndugu yako kwa uso wenyewe Bashasha (Tabasamu)”. [Amepokea Muslim: 6690]

٨١-التزاور في الله: عن أبي هريرة رضي الله عنه، عن النبي ﷺ: ((أن رجلاً زار أخاً له في قرية أخرى ، فأرصد الله له على مدرجه ملكاً (أي: أقعده على الطريق يرقبه) فلما أتى عليه قال: أين تريد؟ قال: أريد أخاً لي في هذه القرية. قال: هل لك عليه من نعمة تربه؟ قال: لا ، غير أني أحبيته في الله عز وجل ، قال: فإنني رسول الله إليك ، بأن الله قد أحبك كما أحببته فيه)) [رواه مسلم: ٦٥٤٩]

81- Kutembeleana kwa ajili ya Allah:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-kutoka kwa Nabii –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- “Hakika mtu mmoja alimtembelea ndugu yake katika kijiji kingine, Allah alimuwekea Malaika njiani (akimsubiri), alipo mfikia akamuuliza: Wapi unakusudia? Akasema: Namkusudia ndugu yangu kwenye hiki kijiji, akamuuliza: Kuna neema yeyote unaitaraji kwake? Akasema: Hapana! Isipokuwa mimi ninampenda kwa ajili ya Allah, akasema: Hakika mimi ni Mjumbe wa Allah kwako, yakwamba Mwenyezi Mungu amekupenda kama ulivyo mpenda kwa ajili yake”. [Amepokea Muslim: 6549]

٨٢- **إعلام الرجل أخيه أنه يحبه**: عن المقدام بن معدى كرب (رضي الله عنه)،
 أنَّ النَّبِيَّ -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَهُ وَعَلَّمَهُ- قَالَ: ((إِذَا أَحَبْتَ أَحَدَكُمْ أَخَاهُ، فَلْيُعْلِمْهُ أَنَّهُ يَحْبُّهُ))
 . [رواه أحمد: ١٦٣٠٣]

82- Muislam kumwambia ndugu yake kuwa anampenda:

Kutoka kwa Miqdam Bin Maad Karbi –Allah amridhie- hakika Nabii –Rehema na Amani zimfikie- amesema: "Mmoja wenu akimpenda ndugu yake na amuambie kuwa anampenda".
 [Amepokea Ahmad: 16303]

٨٣- **رد الشاوب**: عن أبي هريرة -رضي الله عنه-. قال: قال رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَهُ وَعَلَّمَهُ-
 ((الشاؤب من الشيطان، فإذا شاء ب أحدكم فليبرده ما استطاع،
 فإن أحدكم إذا قال: ها، ضحك الشيطان)) [متفق عليه: ٣٢٨٩ - ٧٤٩٠].

83- Kuzuia Miayo:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie- amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah zimshukie- : "Kupiga miayo husababishwa na Shetani, akipiga miayo mmoja wenu, basi na aizue kiasi awezavyo, hakika mmoja wenu atakapo sema: Haa! Shetani

anacheke”. [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 3289,7490]

٤-إحسان الظن بالناس: عن أبي هريرة رضي الله عنه ، أنَّ رسول الله صلوات الله عليه وسلام قال: ((إياكم والظن، فإنَّ الظن أكذب الحديث)) [متفق عليه: ٦٥٣٦-٦٠٦٧]

84-Kuwadhania watu dhana njema:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-Hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ya Allah ziwe juu yake- amesema: “Jiepusheni na dhana (kuwadhania watu vibaya), hakika dhana ni mazungumzo ya uongo zaidi”. [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 6067,6536]

٥-تعاونة الأهل في أعمال المنزل: عن الأسود قال: سألتُ عائشة رضي الله عنها - ما كان النبي صلوات الله عليه وسلام يصنع في بيته؟ قالت: ((كان يكون في مهنة أهله (أي: خدمتهم) ، فإذا حضرت الصلاة خرج إلى الصلاة)). [رواه البخاري: ٦٧٦]

85- Kumsaidia mke kazi za nyumbani:

Kutoka kwa Al-as-wad amesema: Nimemuuliza Aisha –Allah amridhie- Ni yapi aliyo kuwa anayafanya Mtume nyumbani kwake? Akasema:

"Alikuwa ni mwenye kuitumikia familia yake, ukifika wakati wa swala anatoka". [Amepokea Bukhary: 676]

٨٦- سُنْنَةِ الْفَطْرَةِ: عن أبي هريرة -رضي الله عنه- قال: قال رسول الله ﷺ: ((الفطرة خمس، أو خمس من الفطرة: الختان ، والاستحداد (حلق شعر العانة)، ونتف الإبط، وتقليم الأظفار ، وقص الشارب)) [متفق عليه: ٥٨٨٩ - ٥٩٧] .

86-Sunna za maumbile:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : "Mambo ya kimaumbile yapo matano, au mambo matano ni katika maumbile ya kibinadamu: Hitani, Kunyoa sehemu za siri, Kunyofoa nywele kwapa, Kukata kucha, na Kupunguza Masharubu". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 5889,597]

٨٧- كَفَالَةُ الْيَتَمِّ: عن سهيل بن سعد -رضي الله عنه-، عن النبي -صلوات الله عليه وآله وسلامه- قال: ((أنا وكافل اليتيم في الجنة هكذا)). وقال بإصبعيه السبابية والوسطى . [رواه البخاري: ٦٠٠٥]

87- Kmulea mtoto yatima:

Kutoka kwa Sahli Bin Saad –Allah amridhie-kutoka kwa Nabii –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: “Mimi na mwenye kumlea mtoto yatima, tutakuwa peponi kama hivi” akawa anaashiria kwa vidole vyake viwili cha Shahada na cha kati. [Amepokea Bukhary: 6005]

٨٨ -**تجنب الغضب**: عن أبي هريرة رضي الله عنه، أن رجلاً قال للنبي صلوات الله عليه: أوصني ، قال: ((لا تغضب)). فردد مراراً ، قال: ((لا تغضب))

[رواه البخاري: ٦١١٦]

88- Kujierepusha na hasira:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-hakika mtu mmoja alisema kumuambia Mtume –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : Niusie! Akasema: “Usikasirike” akarejea mara nyingi, akasema: “Usikasirike”. [Amepokea Bukhary: 6116]

٨٩ -**البكاء من خشية الله**: عن أبي هريرة رضي الله عنه، عن النبي صلوات الله عليه. قال: ((سبعة يظلمهم الله في ظله، يوم لا ظل إلا ظله ... وذكر منهم: ورجل ذكر الله خالياً ففاضت عيناه)) [متفق عليه: ٦٦٠-١٠٣١].

89- Kulia kwa ajili ya Allah:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-kutoka kwa Nabii –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: "Watu saba, watafunkwa na Allah –Mtukufu- katika kivuli chake, siku ambayo haina kivuli isipokuwa kivuli chake: akamtaja katika hao: na Mtu aliye mkumbuka Allah akiwa faragha, kisha yakamtiririka machozi". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 660,1031]

٩٠-الصدقة الجارية: عن أبي هريرة ﷺ، أن رسول الله - ﷺ -
قال: ((إِذَا ماتَ الْإِنْسَانُ انْقَطَعَ عَمَلُهُ إِلَّا مِنْ ثَلَاثَةِ: إِلَّا مِنْ
صَدَقَةٍ جَارِيَةٍ ، أَوْ عِلْمٍ يَتَفَعَّلُ بِهِ ، أَوْ وَلَدًا صَالِحًا يَدْعُو لَهُ)) [رواه
مسلم: ٤٢٢٣]

90- Sadaka yenyе endelevu:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie- Hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: "Anapo kufa mwanadamu matendo yake yote hukatika (huisha), isipokuwa mambo matatu: Sadaka yenyе kuendelea, Elimu yenyе manufaa, au Mtoto mwema atae muombea". [Amepokea Muslim: 4223]

٩١- **بناء المساجد**: عن عثمان بن عفان - ﷺ . قال عند قول الناس فيه حين بني مسجد رسول الله ﷺ : إنكم أكثرتم وإنى سمعت النبي ﷺ يقول: ((من بني مسجداً . قال بُكير: حسبت أنه قال: يتغى به وجه الله - بني الله له مثله في الجنة)) [متفق عليه: ٤٥٠ - ٥٣٣]

91- Kujenga Misikiti:

Kutoka kwa Uthmani Bin Afani –Allah amridhie-alisema, pale walipo sema watu wakati yeye alipotaka kuujenga Msikiti wa Mtume –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : "Hakika ninyi mmezidisha maneno, mimi nilimsikia Nabii –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake-akisema: Mwenye kujenga Msikiti, Akasema Bukayr: Nadhania kuwa alisema: Akawa anatafuta Radhi za Allah, basi Allah atamjengea mfano wake peponi". [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 450,533]

٩٢- **السماحة في البيع والشراء**: عن جابر بن عبد الله رضي الله عنهما ، أن رسول الله ﷺ . قال: ((رحم الله رجالاً سمحوا إذا باع ، وإذا اشتري ، وإذا اقتضى)) [رواية البخاري: ٢٠٧٦]

92- Kufanya wepesi katika kuuza na kununua:

Kutoka kwa Jabir Bin Abdillahi –Allah awaridhie-Hakika Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- amesema: "Allah amemrehemu mtu ambae anafanya wepesi anapo uza, na anapo nunua, na anapo dai (Deni)". [Amepokea Bukhary 2076]

٩٣- إِزَالَةُ الْأَذى عَنِ الطَّرِيقِ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ، أَنَّ رَسُولَ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ قَالَ: ((بَيْنَمَا رَجُلٌ يَمْشِي بِطَرِيقٍ، وَجَدَ غُصْنًا شَوْكًا عَلَى الطَّرِيقِ، فَأَخْرَهُ، فَشَكَرَ اللَّهُ لَهُ، فَغَفَرَ لَهُ)) [رواه مسلم: ٤٩٤٠]

93- Kuondosha Maudhi njiani:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-kutoka kwa Nabii –Rehema na Amani ziwe juu yake- amesema: "Wakati mtu anapo tembea njiani, akaona tawi lenye miba njiani, kisha akalitoa, basi Allah anamkulalia tendo lake hilo, na anamsamehe". [Amepokea Muslim: 4940]

٩٤- الصَّدَقَةُ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: قَالَ، قَالَ رَسُولُ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((مَنْ تَصَدَّقَ بَعْدَ تَمْرِيدٍ مِّنْ كَسْبٍ طَيِّبٍ، وَلَا يَقْبَلُ اللَّهُ إِلَّا

الطيب، فإن الله يتقبلها بيمنه ، ثم يربيها لصاحبها كما يربى أحدكم فلوة حتى تكون مثل الجبل)) [متفق عليه: ١٤١٠ - ١٠١٤]

94- Kutoa Sadaka:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-amesema” kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- : “Atakaye toa Sadaka kiasi cha Tende moja tu, kutokana na chumo la halali, na hakubali Allah, isipokuwa mambo mazuri, Hakika Allah ataipokea hiyo kwa mkono wake wa kuume, kisha atailea hiyo kwa ajili ya yule aliye itoa, kama anavyo lea mmoja wenu ndama wa Ngamia wake, mpaka itakuwa (sadaka) kama Mlima” [Imeafikiwa usahihi wake na Imam Bukhari na Muslim : 1410,1014]

٩٥- الإكثار من الأعمال الصالحة في عشر ذي الحجة: عن بن عباس رضي الله عنهما ، عن النبي ﷺ، أنه قال: ((ما العمل في أيام أفضل منها في هذه يعني أيام العشر.)) قالوا: ولا الجهاد؟ قال: ((ولا الجهاد، إلا رجل خرج يخاطر بنفسه وماله فلم يرجع بشيء)) [رواوه البخاري: ٩٦٩]

95- Kutenda mema kwa wingi, Siku kumi za Mfungo tatu:

Kutoka kwa Ibn Abasi –Allah amridhie- kutoka kwa Mtume –Rehema na Amani ziwe juu yake-amesema: "Hakuna matendo (mema) kwenye siku bora zaidi kuliko siku hizi (anakusudia siku kumi), wakasema: Hata Jihadi? Akasema: Hata Jihadi, isipokuwa mtu aliye toka akaitia hatarini nafsi yake, na mali yake, kisha hakurudi na chochote". [Amepokea Bukhary: 969]

٩٦ - قُتِلَ الْوَزْغُ: عَنْ أَبِي هُرَيْرَةَ - رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُ - قَالَ: قَالَ رَسُولُ اللَّهِ عَلَيْهِ السَّلَامُ : ((مِنْ قُتْلِ وَرَغَافٍ فِي أُولَى ضَرَبَاتٍ كَتَبَتْ لَهُ مِئَةٌ حَسَنَةٌ، وَفِي الثَّانِيَةِ دُونَ ذَلِكَ، وَفِي الثَّالِثَةِ دُونَ ذَلِكَ)) [رواه مسلم] [٨٥٤٧]

96- Kuua mjusi:

Kutoka kwa Abuu Hurayra –Allah amridhie-amesema: kasema Mjumbe wa Allah –Rehema na Amani ziwe juu yake-: "Atakaye muua Wazagh (Mjusi) katika pigo la kwanza, ata andikiwa mema mia moja, na akiua kwa pigo la pili, (ata andikiwa) chini yake, na akiua kwa pigo la tatu (ata andikiwa) chini yake". [Amepokea Muslim: 2240]

٩٧- النهي عن أن يُحَدِّث المرء بكل ما سمع: عن حفص بن عاصم -رضي الله عنه- قال: قال رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ: ((كفى بالمرء إثماً أن يُحَدِّث بكل ما سمع)) [رواه مسلم: ٧]

97- Katazo kwa Mtu kukizungumza kila alichokisikia:

Kutoka kwa Hafswi bin Aaswim –Allah amridhie-amesema: amesema Mtume wa Allah –Rehema na Amani za Allah zimshukie- “Inatosha Mtu kupata Dhambi kwa kuzungumza kila alichokisikia” [Ameipokea Muslim: 7]

٩٨- الرَّمَلُ فِي الطَّوَافِ: عن ابن عمر - رضي الله عنهما - قال: ((كان رسول الله -صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّدَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - إذا طاف الطواف الأول، خبَّ (أي: رَمَلَ) ثلاثة ومشي أربعًا ... الحديث)) [متفق عليه: ١٦٤٤ - ٣٠٤٨]

98- Kwenda haraka haraka kwenye kutufu Ka `aba:

Kutoka kwa Ibin Umar –Allah awaridhie-amesema: “Alikuwa Mtume wa Allah –Rehema na Amani za Allah ziwe juu yake- Pindi anapo fanya Ibada ya kutufu Al-ka`aba (kuizunguka) kwa mara ya kwanza (anapo fika makka),

anatembea haraka haraka (mizunguko) mitatu ya mwanzo, na anatembea kawaida (mizunguko) minne ya mwisho...” [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 1644, 3048]

٩٩- احتساب النفقة على الأهل: عن أبي مسعود البدرى رضي الله عنه، عن النبي صلوات الله عليه وآله وسلامه قال: ((إن المسلم إذا أنفق على أهله نفقة ، وهو يكتسبُها ، كانت له صدقة)) [رواه مسلم: ٢٣٢٢]

99- Kutegemea Thawabu katika kuihudumia Familia:

Kutoka kwa Abuu Mas-uud Al-Badriy –Allah amridhie- Amesema: “Hakika ya Muislam atakapo toa huduma yeyote kwa Fmilia yake na huku akitegemea malipo kwa Allah, itakuwa ni Sadaka yake” [Ameipokea Muslim: 2322]

١٠٠ - المداومة على العمل الصالح وإن قل: عن عائشة رضي الله عنها، أنها قالت: سُئل رسول الله ﷺ: أي الأعمال أحب إلى الله؟ قال: ((أدومها وإن قل)) [متفق عليه: ٦٤٦٥ - ١٨٢٨]

100- Kudumu kwenye matendo mema japo yawe madogo:

Kutoka kwa Aisha –Allah amridhie- hakika amesema: Aliulizwa Mtume wa Allah –Rehema na Amani za Allah zimshukue-: Ni matendo gani yanayo pendeza zaidi kwa Allah? Akasema: "Ni yenye kudumu, japo kuwa ni machache" [Imeafikiwa usahihi wake na Bukhari na Muslim: 6465, 1828]

Na amemrehem Allah na amempa amani na ambariki Nabii wetu Muhammad, na Familia yake na Masswaaba zake wote.

YALIYOMO:

UTANGULIZI	2
SUNNA ZA KULALA	3
1-Kulala na udhuu:	3
2-kuletaTakbira na Tasbiha wakati wa kulala:.....	4
3-Kusoma Surat Al-Ikhlas na Al-Mu'awwidhatayn [Qul Audhu birabbi nnasi na Qul Audhu birabbi Al Falaq] kabla ya kulala:	5
4-Dua wakati wa kuamka kati kati ya usingizi:	6
5-Dua ya kuamka usingizini, imethibiti Dua hii:	7
SUNNAH ZA UDHU NA SALA	8
6- Kusukutua na na kutia maji puan, kwa mchoto mmoja wa maji:	8
7- Kutawadha kabla ya kuoga:.....	8
8- Tashahhud (Dua) baada ya kutawadha:	9
9- Kuhifadhi maji kwa kutumia kwa wastani:	10
10- Kuswali rakaa mbili baada ya kutawadha:	10
11- Kurudia maneno ya Muadhini, kisha kumswalia Mtume -Rehema na Amaani zimfikie:-	11
12- Kupiga mswaki mara kwa mara:	12
13- Kuelekea msikitini mapema:	13
14- Kwenda msikitini kwa miguu:.....	13
15- Kuswali kwa utulivu na taadhima:	14
16- Dua ya kuingia na kutoka msikitini:	15
17- Kuswali hali ya kuweka mbele Sutrah (kinga):....	15
SUTRAH:	16
18- Kukaa kikazi cha Al-Iqaa ,(kukalia miguu miwili) kati ya Sijda mbili:	16

19- kukaa kikazi cha (Al-Tawwaruku) katika Tashahhud ya pili:	17
20- Kuomba dua nyingi kabla ya kutoa salam:	18
21- Kutekeleza Sunnah za kawaida (kabla na baada ya swala):	18
22-Swala ya Dhuha:	19
23- Qiyaam al-Layl (swala ya usiku):	20
24- Swalah ya Witr:	20
25- Kuswali swala za Sunna nyumbani:	21
26- Kuswali na viatu vikiwa visafi:	21
27- Kuswali katika Msikiti wa Qubaa:	22
28- Kukaa sehemu ya kuswali baada ya Swalah ya alfajiri mpaka jua linapochomoza:	22
29- Kuoga siku ya Ijumaa:	23
30- Kwenda mapema kwenye Swalah ya Ijumaa:	23
31- Kutafuta muda wa kujibiwa dua siku ya Ijumaa:	24
32- Kwenda kwenye swala ya Idi kwa njia moja, na kurejea kwa njia nyingine:	25
33- Swala ya Maiti:	25
34- Kuzuru makaburi:	26
35- Swala ya Istikharah (kuomba kheri):	27
SUNNA ZA KUFUNGA	28
36-Kula Daku:	28
37-Kuharakisha kufuturu, mara baada ya kuzama Jua:	28
38-Swala ya usiku mwezi wa Ramadhan:	29
39-Kukaa Itikaaf katika mwezi wa Ramadhan, hasa kwenye kumi la mwisho:	30
40-Kufunga siku sita, mwezi wa Mfungo mosi:	30

41-Kufunga siku tatu kila mwezi:	31
42-Kufunga siku ya Arafat:	31
43-Kufunga siku ya Aashuraa:	32
SUNNA ZA SAFARI	33
44-Kuchagua kiongozi mkiwa safarini:	33
45-Kusoma Takbir (Allahu akbar) wakati wa kupanda (mlima), na Tasbihi (Subhana Allah) wakati wa kushuka:	33
46-Dua ukifika katika nyumba yejote:	34
47-Kufikia Msikitini, akirudi kutoka safari:	35
SUNNA ZA MAVAZI NA CHAKULA	36
48-Dua wakati wa kuvaan Nguo mpya:	36
49-Kuvaan viatu, kuanza mguuu wa kulia:	37
50-Kusoma Bismil-lahi wakati wa kula:	37
51-Kumshukuru Allah baada ya kula na kunywa:	38
52-Kukaa wakati wa kunywa:	38
53-Kusukutua baada ya kunywa Maziwa:	39
54-Kuto kikitia kasoro chakula:	39
55-Kula kwa (kutumia) vidole vitatu:	40
56-Kunywa na kujitibu kwa Maji ya Zamzam:	40
57-Kula siku ya Eid Al-fitri kabla ya kwenda kuswali:	41
DHIKRI (KUMTAJA ALLAH) NA DUA	42
58-Kusoma sana Qur-an:	42
59-Kusoma Qur-an kwa sauti nzuri:	42
60-Kumtaja Allah kwa kila hali:	43
61-Kumsabihi Allah (Subhana Allah):	44
62-Kumuombea Dua aliye piga chafya:	45
63-Dua ya kumuombea mgonjwa:	45

64-Kuweka mkono sehemu yenyeye maumivu, pamoja na kuomba Dua:	46
65-Dua inayo ombwa kwa kusikia sauti ya Jogoo, kujilinda kwa Allah kwa kusikia sauti ya Punda:.....	47
66- Dua wakati wa kunyesha mvua:	47
67-Kumtaja Allah wakati wa kuingia nyumbani:	48
68-Kumtaja Allah kwenye kikazi:	49
69-Dua wakati wa kuingia chooni:.....	49
70-Dua wakati wa kuvuma upopo mkali (kimbunga):	50
71-Kuwaombea Dua waislam, kwa siri:.....	51
72-Dua wakati wa matatizo:	51
73-Kusalimiana:	52
SUNNA MBALI MBALI	53
74-Kutafuta Elimu:.....	53
75-Kupiga hodi mara tatu, kabla ya kuingia:.....	53
76-Kumrambisha mtoto mchanga kitu kitamu:	54
77-Kumfanyia Akika mtoto:.....	55
78-Kufunua sehemu ya mwili ili ipatwe mvua:	55
79-Kumtembelea mgonjwa:	56
80-Kutabasamu:	56
81-Kutembeleana kwa ajili ya Allah:.....	57
82-Muislam kumwambia ndugu yake kuwa anampenda:.....	58
83-Kuzuia Miayo:.....	58
84-Kuwadhania watu dhana njema:	59
85-Kumsaidia mke kazi za nyumbani:.....	59
86-Sunna za maumbile:	60
87-Kmulea mtoto yatima:.....	61

88-Kujiepusha na hasira:	61
89-Kulia kwa ajili ya Allah:	62
90-Sadaka yenyenye endelevu:	62
91- Kujenga Misikiti:	63
92-Kufanya wepesi katika kuuza na kununua:	64
93-Kuondosha Maudhi njiani:	64
94- Kutoa Sadaka:	65
95-Kutenda mema kwa wingi, Siku kumi za Mfungo tatu:	66
96-Kuua mjisii:	66
97- Katazo kwa Mtu kukizungumza kila alicho sikia:	67
98- Kwenda haraka haraka kwenye kutufu Ka`aba:	67
99- Kutegeomea Thawabu katika kuihudumia Familia:	68
100- Kudumu kwenye matendo mema japo yawe madogo:	69
YALIYOMO:	70